Azimio kwa Uhai wa Viumbe vyote Hai Duniani

DIBAJI

Dunia ni maumbile yenye uhai yanayoendelea kusitawi. Kila kiumbe chenye uhai duniani ni muhimu kama kimojawapo cha vipuri vinavyounda maumbile haya. Kutokana na dhana hii, sisi kama wanadamu, kibinafsi lazima tuzingatie umuhimu wa kuelewa zaidi kwamba sisi sote ni jamii ya dunia yenye viumbe vya uhai na kwamba sisi tuna wajibu mmoja na jukumu kwa ajili ya maisha siku za usoni ya dunia yetu.

Kila mtu kati yetu ana wajibu wa kutimiza shabaha ya kusitawisha dunia yetu, na kwa ajili ya kuleta amani ulimwenguni kila mmoja kati yetu lazima ajitwike jukumu na kuwajibika. Hadi hapo wakati huu wa sasa, hapa duniani hakuna watu ambao wamekuwa wakiridhika kikamilifu katika maisha yao. Tumekuwa tukikabiliwa na mizozo kote duniani kwa sababu ya mashindano ya kujipatia maliasili na ardhi ambazo zote mbili akiba zao zina kikomo. Jambo hili limekuwa likitoa athari mbaya dhidi ya mazingira ya dunia nzima.

Kwa kuwa tumekwisha ingia katika enzi mpya ya miaka ya elfu mbili, zaidi ya kitu kingine cho chote, utekelezaji wa kuwepo kwa amani duniani unategemea hasa kuzindika kwa dhamiri njema ya kila mmojawapo wa jamii ya wanadamu juu ya jambo hili. Siku hizi, jambo muhimu linalolazimishwa kutekelezwa ni kwamba kila mwanadamu atimize jukumu la kuleta amani na upatanifu moyoni mwake binafsi. Sisi sote tunapewa shabaha hii muhimu ya pamoja ambayo inatupasa kuitekeleza kikamilifu. Kuwepo kwa amani duniani kutafanikiwa tu wakati kila mmojawapo wa wanadamu atakapoweza kuzingatia juu ya shabaha hii muhimu ya pamoja, na tena sisi sote tutakapoweza kuunga mikono kwa pamoja kwa ajili ya kutekeleza madhumuni haya yetu ya pamoja.

Hadi hapo, kama tukitaja juu ya fani za mamlaka, utajiri, umaarufu, maarifa, teknolojia na elimu, ulimwengu umekuwa ukigawanyika kati ya watu binafsi, mataifa na mashirika, na hata kati ya makundi hayo, unagawanyika kati ya wale wenye kumiliki fani hizo na wale wengine wasiokuwa nazo fani hizo. Na vilevile kumekuwwepo hitilafu kadhaa kati ya wale watoaji misaada na wapokeaji, na pia kati ya wasaidizi na wale waliosaidiwa.

Hapo basi tunatangaza azimio letu tukiwa tunavuka njia panda hizi za masuala hayo yote yaliyoko katika pande hizo mbili za kukabiliana na hitilafu mbalimbali, tukiwa tumezatiti dhana mpya kabisa ambayo itatoa huduma kama msingi wetu wakati tunapoanza shughuli za kujenga ulimwengu wenye amani.

KANUNI ZA JUMLA

Katika enzi mpya, wanadamu tunapaswa kusonga mbele kuelekea ulimwengu wenye maelewano, yaani ulimwengu ambako kila nchi na kila mwanadamu atakuwa na uhuru wa kuonyesha tabia yake binafsi, huku akiishi vizuri na akishirikiana pamoja kirafiki pamoja na wenzake na viumbe vingine vyote vinavyoishi duniani. Ili kutekeleza shabaha hii ya siku za usoni, tumetunga kanuni zifuatazo za mwongozo.

1. Kutoa heshima kwa uhai

Tutaunda ulimwengu chini ya msingi wa upendo na upatanifu ambamo uhai wa viumbe vyote unaheshimiwa.

2. Kuheshimu tofauti za kila aina

Tutaunda ulimwengu ambamo jamii tofauti, makabila, dini, utamaduni、mila na desturi zote hizo zinaheshimiwa. Ulimwengu lazima uwe mahali penye uhuru kutoka katika hali za ubaguzi au mapambano, kijamii, kimwili na kimoyo na tena uwe mahali ambako hitilafu zilizoko sasa zinatambuliwa vyema na kufurahiwa.

3. Shukurani kwa maumbile yote na kuishi pamoja kwa kushirikiana nayo.

Tutaunda ulimwengu ambamo kila mtu azingatie kwamba tunaweza kuishi kupitia neema ya maumbile, na kuishi pamoja kwa kushirikiana na maumbile, tukionyesha shukurani zetu kwa wanyama wote, mimea na viiumbe vingine vyote vyenye uhai vilivyoko duniani..

4. Upatanifu baina ya roho na vitu visivyo na uhai

Tutaunda ulimwengu chini ya msingi wa kuwa na uwiano wa upatanifu baina ya kuweka mizani kati ya kuthamini vitu na ustaarabu wa kiroho.. Lazima tuondokane na hali ya kuwa na dhamiri ambayo inathamini sana vitu kupita kiasi ili kuikaribisha roho safi ichanue vizuri nyoyoni mwa wananadamu wote. Lazima
tujenge ulimwengu ambamo siyo tu kuwemo kwa vitu tele vyenye thamani bali pia ukwasi wa kiroho unathaminiwa inavyostahiki.

MAZOEZI

Tutasimamisha nguzo za kanuni hizi zishughulikiwe zikiongozwa na misingi ifuatayo:

Kama mtu binafsi:

Hatuna budi kusonga mbele kupitia enzi ambamo mamlaka na jukumu ziko mikononi mwa mataifa, makabila na dini kuelekea enzi mpya ambapo mtu binafsi anaweza kujitegemea akiwa anapewa heshima.

Sisi tunatazamia “Enzi ya mtu binafsi” lakini hii inamaanisha siyo hali ya kutilia mkazo nadharia ya ubinafsi, bali enzi ambapo kila mtu binafsi yuko tayari kukubali kutimiza jukumu na kutekeleza wajibu wake kibinafsi kama mmojawapo wa wanachama wa kujitegemea katika jamii ya wanadamu.

Kila mtu kati yetu atekeleze wajibu wetu ulio muhimu kwa ajili ya kushamirisha upendo, kuchochea maelewano na shukurani katika nyoyo zetu sisi wenyewe na kufanya hivyo tutaleta upatanifu katika kila pembe ya ulimwengu.

Katika fani zetu zilizo maalumu:
Tutaunda utaratibu wa ushirikiano ambako hekima zinakusanywa kwa pamoja kwa ajili ya kutekeleza shabaha yetu, na hekima hizo nyingi zinatokana na maarifa ya kifundi, ujuzi na uwezo mwingi katika fani mbalimbali, kama vile elimu, sayansi, utamaduni na sanaa, pamoja na dini, falsafa, siasa na uchumi.

Kuhusu kizaji cha vijana:
Katika karne ya ishirini, wazazi, waalimu na jamii, wote hawa walikuwa waalimu wa kuwafundishia watoto, na watoto walikuwa siku zote wako katika upande wa kufundishwa. Lakini katika karne hii ya ishirini na mmoja, watu wazima wanapaswa kujifunza kutoka chemchemi ya tabia nzuri za watoto walizo nazo, kama vile usafi wa nyoyo zao, nuru yao ya kuvutiwa, uchangamfu, hekima na kipaji, ili wapalilie nyoyo zao na kuinua hali yao kibinafsi. Kizazi cha vijana kitabeba wajibu muhimu sana wa kusakifu misingi ya ufanisi mwema na kufungua milango ya kesho bora.

Amani na iwepo duniani!